# Mabasi 60 mwendokasi yaazimwa yahudumie njia ya Kimara

Na Tatu Mwakabana

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila amesema takribani mabasi 60 ya mwendokasi yameazimwa kutoka njia ya Mbagala yahudumie wananchi kwenye njia ya Kimara kwenda katikati ya mji.

Chalamila alitoa ahadi hiyo alipotembelea Kituo cha mabasi ya mwendokasi cha Kimara jana.

"Muda wowote kuanzia kesho tunatarajia Mungu akijalia tutatue jambo hili angalau kwa nusu, wakati tukiwa tunasubiri mabasi ya muda mrefu yatakapofika," alisema.

Chalamila alisema kabla ya wiki hii kumalizika, serikali itakuwa imepeleka mabasi yasiyozidi 60 ya Kampuni ya Mofat ambayo yameletwa kwa ajili kutoa huduma katika Barabara ya Kilwa.

"Tumekwishakaa na kampuni inayotoa huduma Barabara ya Kilwa, ambayo mabasi yake yamekwishafika ili angalau sasa baadhi ya mabasi yaanze kutoa huduma kwenye Barabara hii ya Morogoro. Halafu mabasi ya njia hii yatakapofika, mabasi haya tuliyoyaomba yataendelea na safari nyinginezo," alisema.

Chalamila aliahidi kufanyia kazi kwa haraka mpango wa mabasi ya kawaida, ili yaongezeke Barabara ya Morogoro lakini si kwa kutumia njia ya mwendokasi kwa kuwa mfumo wake hauruhusu kutumia mabasi ya kawaida.

Alisema haiwezekani kuruhusu daladala za kawaida kutumia barabara za mwendokasi kwa sababu za kiusalama. Kuna tofauti ya kimuundo wa mabasi ya mwendokasi na daladala.

Chalamila alisema utaratibu wa utengenezaji mabasi ya mwendokasi huwa ni wa kuagiza kulingana na vipimo vya barabara na mahitaji ya eneo husika la mradi.

CamScanner

Uhuru Alhamisi Oktoba 2 2025 Pg 3

# RC Chalamila ashusha presha wasafiri mabasi mwendokasi

Na ATHNATH MKIRAMWENI

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amewahakikishia wananchi wa Kimara kuwa, ndani ya wiki hii, mabasi ya mwendokasi, yataongezwa katika njia hiyo, kupunguza adha ya usafiri, tayari serikali imeingia makubaliano na kampuni binafsi.

Kauli hiyo, aliitoa jijini Dar es Salaam jana alfajiri, alipotembelea kituo cha mabasi ya mwendokasi cha Kimara, kufuatia serikali ya mkoa huo, kubaini adha kubwa wanayoipata wananchi wanaotumia usafiri huo, hususan wanaotoka maeneo ya Mbezi na Kimara kuingia katikati ya jiji

Akizungumza katika ziara hiyo, Chalamila alisema kabla ya kumalizika wiki hii, serikali imekusudia kupeleka mabasi machache, huku wakitafuta suluhisho la kudumu.

Chalamila, alisema zaidi ya mabasi 200, yamepakiwa kwenda Dar es Salaam kutoa huduma hiyo kupitia mkandarasi mpya.

Pia, kutokana na ombi la wananchi waliojitokeza katika ziara hiyo kutaka mabasi ya kawaida kuruhusiwa kupeleka wananchi katikati ya jiji kupitia njia ya mwendokasi ama njia ya kawaida isipokuwa ya mwendolasi, Chalamila aliahidi kuufanyia kazi mpango huo haraka.

"Nitalifanyia kazi kwa haraka ombi hili la mabasi ya kawaida yaongezeke, ingawa si kwa kutumia njia ya mwendokasi kwa kuwa, mfumo wake hauruhusu kutumia mabasi ya kawaida,"alisema.

Vilevile, alisema mtoa huduma wa sasa katika njia ya Kimara, ataondolewa mara moja baada ya mabasi hayo mapya kuwasili.

Alisema zabuni hiyo, itakabidhiwa kwa mtoa huduma mwingine mwenye uwezo wa kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi.

"Wiki hii kabla haijaisha kutakuwa na mabasi mapya machache yatakayoingia wakati tunatafuta suluhu ya kudumu. Huyu mtoa huduma wa sasa tunamwondoa na tunamleta mpya," alisema.

Pia, Chalamila aliwahakikishia wakazi wa Dar es Salaam kuwa, serikali itaendelea kuboresha huduma za usafiri wa umma kwa kuhakikisha upatikanaji wa mabasi ya kutosha na kuimarisha mfumo wa mwendokasi kwa wananchi wote.

CamScanner

# Ndani ya Habari

**HABARI:** Ukata Jumuiya Afrika Mashariki unavyoumiza wafanyakazi UK 12

**UCHUMI:** Faida ya miamala ya kidijitali na hatari zake UK 15

## Mwendokasi bado kero Dar

**Mintanga Hunda na Nasra Abdallah,** Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Wakati wananchi wakiendelea kulazimika kusubiri muda mrefu kupata huduma ya usafiri wa mabasi yaendayo haraka maarufu mwendokasi, Serikali mkoani Dar es Salaam imetoa taarifa ya namna inavyoshughulikia kero hiyo, ambayo wengi hulazimika kuyapanda kwa kugombea.

Asubuhi ya jana Oktoba mosi, 2025, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila alifanya ukaguzi kwenye baadhi ya vituo vya mabasi hayo na kushuhudia kero wanazokabiliana nazo wananchi.

Akiwa kituo kikuu cha Kimara Mwisho, wananchi walikuwa katika hekaheka za kugombea mabasi machache yanayofanya safari, baadhi walisikika wakiimba: "Hatuitaki CCM, hatuitaki CCM."

Chalamila alipowatuliza na kuwasihi kuwa shida hiyo itakwisha hivi karibuni, baadhi ya abiria walikuwa wakiendelea kugombea kuingia kwenye basi, huku wakiendelea kuimba hata pale walipokuwa ndani ya basi.

Kwa wale waliomsikiliza Chalamila, wakiwamo wanaotoka Mbezi, ambao hushushwa Kimara Mwisho ili kuendelea na safari, walieleza kero inayowakabili ya kusubiri mabasi muda mrefu, huku wakiyapanda kwa taabu kwa kuwa hulazimika kugombea kuingia ndani na wakati mwingine hushushwa, ili mlango uweze kufungwa.

Chalamila akizungumza na wananchi hao alisema: "Leo (jana) saa 11:00 alfajiri nimefanya ziara katika baadhi ya vituo vya mabasi yaendayo haraka kuanzia Gerezani hapa Kimara na nitamalizia Mbezi. Hapa tupo na Jeshi la Polisi – RPC (Kamanda wa Polisi Mkoa) na RTO (Mkuu wa Trafiki Kinondoni)."

Alisema amefanya safari kwenye vituo hivyo baada ya kuona video fupi zikionyesha watu wanagombea kuingia kwenye mabasi.

"Nikiri kuwa mabasi yameshapungua sana kutoka kwenye idadi yake mpaka yalivyo sasa. Hivi tunapoongea mabasi ya kampuni ya Udart yanayotoa huduma hayafiki hata 40. Hayo yanayotoa huduma ndiyo yenye uhafadhali," alisema.

Mradi wa BRT katika barabara hiyo ulilenga kuwa na mabasi 305. Hata hivyo, mpaka ulipoanza kufanya kazi mwaka 2016 ulikuwa na mabasi 140.

Mwaka 2021 mabasi 70 yaliyokuwa yamezuiwa baada ya kutokamilika taratibu za kuingizwa nchini, yaliruhusiwa kuingia barabarani, hivyo kufanya idadi kufika mabasi 210, ingawa wakati huo mengine yalikwishaharibika kutokana na mafuriko na sababu nyingine.

> **"Tumeona baadhi ya clip wakisema hatuitaki CCM, hatumtaki mama, naomba niwaeleze ukweli kwamba hizi ni hasira za muda mfupi. Mara Serikali itapoingiza mabasi haya naamini kabisa unaposema leo huitaki CCM sawa, usipoitaka ndiyo mbadala wa mabasi? Hapana, kwani lazima tutatue mambo haya kwa kutumia kauli moja, kwa ushirikiano kwa kujua kwamba, hatuna nchi nyingine."**
> Mkuu wa Mkoa, Albert Chalamila



Abiria wakisukumana kuingia kwenye basi la mwendokasi katika kituo cha la Kimara, Dar es Salaam jana.

Chalamila alisema kutokana na hali hiyo, amepatikana mtoa huduma mwingine nje ya Udart (Kampuni ya Uendeshaji Usafiri wa Haraka) katika njia hiyo, hivyo mabasi yatakayoingia yatakuwa tofauti na Udart.

Hatua hiyo, alisema inalenga kumpata mtu mwingine mwenye nguvu, uwezo na teknolojia ili kuongeza ushindani katika utoaji huduma.

"Barabara ya Kilwa, tulisema ifikapo Agosti 15, mwaka huu kutakuwa na mabasi mapya yatakayoingia kutoka nchini China. Ni kweli ilipofika siku hiyo mabasi yote yaliwasili kwenye Bandari ya Dar es Salaam, baada ya hapo yalianza kushughulikiwa mambo mengine ikiwapo kodi," alisema.

Alisema mabasi ya Barabara ya Kilwa yaliyowasili ni 151 ambayo yapo kwenye karakana iliyopo Mbagala yakisubiri vibali vyote vikamilike ili yaingie barabarani.

"Mungu akijalia wiki hii au ijayo mabasi ya Mofat (kampuni ya wazawa iliyopewa zabuni) yatakuwa yaanza kufanya kazi. Kilichopo kwenye barabara hii (Morogoro) kwa kuwa mabasi ni machache na uhitaji ni mkubwa, tulishakaa na kampuni ya Mofat ili angalau baadhi ya mabasi yaanze kutoa huduma kwenye barabara hii, halafu mabasi ya Morogoro Road yatapokuwa yamefika basi haya ya Mofat yataendelea na route nyingine."

Chalamila alisema: "Suala la msingi ni mabasi haya yatakuwa yamefika kwenye barabara hii muda wowote kuanzia kesho (leo). Mungu akijalia tuwe tumetatua angalau nusu ya tatizo hili, huku tukisubiri mabasi ya kudumu."

Alitoa rai kwa wananchi akiwaomba msamaha na kuwataka radhi akisema: "Najua hakuna Serikali yenye lengo la kutenda uovu kwa wananchi wake na kuwataka wahangaike."

Alisema huduma zinatolewa kwa ubia kati ya Serikali na sekta binafsi: "Kwa hiyo nimeona ndugu zangu niwaeleze haya Watanzania wa Dar es Salaam waendelee kuvumilia."

"Tumeona baadhi ya clip wakisema hatuitaki CCM, hatumtaki mama, naomba niwaeleze ukweli kwamba hizi ni hasira za muda mfupi. Mara Serikali itapoingiza mabasi haya naamini kabisa unaposema leo huitaki CCM sawa, usipoitaka ndiyo mbadala wa mabasi? Hapana, kwani lazima tutatue mambo haya kwa kutumia kauli moja, kwa ushirikiano kwa kujua kwamba, hatuna nchi nyingine," alisema.

Chalamila alisema mabasi hayo yalipoanza miaka mingi nyuma watu wengi waliyabeza na kuonyesha kuwa ni mradi wa aina gani, lakini siku zinavyozidi kwenda wanagundua mabasi hayo ni msaada mkubwa.

"Tunachokiona leo mahitaji ni makubwa, ingekuwa siyo kitu kizuri, usingemuona mtu anasukumana mlangoni kwenye hayo mabasi. Kwa hiyo hakuna namna, Serikali lazima isimamie mradi huo," alisema na kuongeza:

"Katika hili nashukuru sana Waziri Mkuu wetu amekesha usiku na mchana kuendesha vikao kuona namna ambavyo tunaweza kutatua jambo hili. Zitakuja mamlaka zingine za juu kuja kuwaeleza Watanzania na pengine wasiwe na wasiwasi kuhusu huduma hii ya mabasi yaendayo kwa haraka."

Watendaji wa Mofat hawakupatikana kuzungumzia makubaliano hayo.

Alipotafutwa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (Dart), Dk Athuman Kihamia kutoa ufafanuzi kuhusu kauli ya Chalamila alisema:

"Nadhani kwa kuwa Mkuu wa Mkoa ndiye aliyeongea ni vema akatafutwa yeye kulifafanua zaidi kama hamjalielewa au hata msaidizi wake, lakini kwa mimi sina cha kuongea juu ya hilo."

### Huduma Mbagala

Huduma ya usafiri huo katika Barabara ya Kilwa ilipangwa kuanza Septemba baada ya mabasi 151 kuwasili nchini lakini hilo halikufanyika, moja ya sababu ilitajwa ni kutokuwapo mageti janja kwa ajili ya malipo.

Mabasi hayo yatafanya safari kati ya Mbagala-Gerezani, Mbagala –Kivukoni na Mbagala- Morocco.

Mradi huo wa awamu ya pili utakaotekelezwa ukiwa wa pili baada ya ule wa Kimara ulioanza mwaka 2016, utaendeshwa na kampuni ya wazawa ya Mofat kwa mkataba wa miaka 12. Kampuni hiyo inatarajiwa kuingiza nchini mabasi 255.

Jana *Mwananchi* ilishuhudia mashine zikiwa zimeshafungwa kwenye mageti janja ya vituo vingi, huku kazi ikiendelea.

Kwenye vituo vya Kamata hadi Mbagala Rangi Tatu kulikuwa na mafundi wakiendelea na kazi, ikiwamo kuvifanyika usafi kwenye vituo.

Baadhi ya wananchi waliozungumza na *Mwananchi,* walisema licha ya kazi zinazoendelea kufanyika, wataamini iwapo huduma itatolewa pale watakapopanda mabasi.

"Kufungwa mashine, kufanywa usafi hakuwezi kutuaminisha kwamba ndiyo huduma zinaanza, isipokuwa tutaamini siku tutakapokuwa ndani ya mabasi," alisema Zuwena Kimweri, mkazi wa Mbagala Rangi Tatu.

Kwa upande wake, Doto Charles, alisema tangu mabasi hayo yaingie nchini takribani mwezi mmoja, wanayaona kituoni tu licha ya wao kutaabika kutokana na adha ya usafiri.

Mabasi 99 yaliwasili nchini Agosti 5 na mengine 52 Agosti 26, 2025. Yote yapo katika karakana ya Mbagala Rangi Tatu.

Mabasi hayo yenye urefu wa mita 18 kila moja yana uwezo wa kubeba abiria 160 na matarajio ya Mofat ni kusafirisha abiria 325,000 hadi 400,000 kwa siku.

Awali, huduma kwa barabara ya Mbagala zilikuwa zianze Septemba mosi, 2025 lakini ilishindikana kutokana na kutokamilika kwa kituo cha kujazia gesi na kufungwa mageti janja yatakayotumika kuchanjia kadi wakati wa kuingia kwenye vituo hivyo.

Lengo ni kuondokana na matumizi ya tiketi, hali ambayo inaaminika itasaidia uhifadhi wa mazingira na kudhibiti upotevu wa mapato.

CamScanner